Maswali

1. Mbona Farao alikuwa na uoga?
2. Mpanga wa Farao wa kwanza ulikuwa nini?
3. Mpango wa Farao wa pili ulikuwa nini?
4. Nani alikuwa anatarajia mtoto?
5. Baada ya Yokebedi kuzaa mtoto mvulana alifanya nini kwa miezi mitatu?
6. Yokebedi alitengeneza nini baada ya kushindwa kuficha mtoto zaidi?
7. Yokebedi alificha mtoto wapi ndani ya kikapu chake?
8. Nani alilinda mtoto?
9. Nani alipata mtoto?
10. Nani alilelea binti mfalme mtoto?
11. Binti mfalme alimuita mtoto eti nani?
12. Nini yenye Musa hakusahau alipokuwa kwa jumba la mfalme?

Majibu

1. Waisraeli walikuwa taifa kubwa na ya nguvu. Wanaweza kuwapiga Wamisri.
2. Farao aliwafanya Waisraeli kuwa na kazi ngumu kama watumwa.
3. Aliamrisha kwamba watoto wavulana wachanga wa Waisraeli wote wauawe.
4. Amramu na Yokebedi walitarajia mtoto.
5. Yokebedi alificha mtoto.
6. Yokebedi alitengeneza kikapu cha majani na akapaka lami.
7. Alificha kikapu chenye mtoto kando ya bahari ndani ya unyasi.
8. Miriamu alilinda mtoto.
9. Binti mfalme alipata mtoto.
10. Yokebedi alilelea binti mfalme mtoto wake.
11. Binti mfalme aliita mtoto eti Musa.
12. Musa hakuwahi kusahau familia yake wakati aliishi kwa jumba la mfalme.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3

12 Musa katika majani

Marejeo

Kutoka 1:8 – 22 na 2:1 – 10

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Amramu na Yokebedi walikuwa na imani kwa Mungu na ilimsaidia mwanao.

Maneno maalum

12.1 Farao mpya + Waisraeli + taifa kubwa + Farao + ogopa + watumwa

12.2 Waisraeli + nguvu zaidi + Farao akasirika + ua watoto wavulana + Amramu na Yokebedi + mtoto mchanga + ficha miezi 3

12.3 Yokebedi + kikapu cha majani + ficha + Miriamu ana linda + binti mfalme + mtoto analia + Miriamu + mlezi + mama

12.4 Binti mfalme + mtoto + Yokebedi + furahi + shukuru Mungu + binti mfalme + mwana + Musa + jumba la mfalme + hakusahau familia.

12.1 Baada ya miaka mingi kulikuwa na Farao mwingine mwenye hakukumbuka vile Yusufu aliwasaidia Wamisri. Baada ya Yakobo na Yusufu kukufa, familia yao ilikua na kukuwa watu wengi. Mungu alikuwa amempa Yakobo jina linguine – Israeli. Familia hiyo waliitwa Waisraeli. Walikua na wakawa taifa kubwa.

Farao mgeni alikuwa na uoga juu ya Waisraeli. Walikuwa wengi sana tena walikuwa wa nguvu. Aliogopa kwamba Waisraeli watakuwa na nguvu kushinda Wamisri. Alikuwa na wasiwasi akifikiria kwamba Waisraeli watawapiga. Farao alikuwa na mpango.

Farao aliwafanya Waisraeli kuwa watumwa wake. Aliwawekea wasimamizi kuwafanyiza kazi ngumu. Walijengea Farao miji mikubwa ya thamani. Wasimamizi waliwachapa mijeledi kama wangelegeza kufanya kazi. Walifanya maisha yao kuwa ngumu.

12.2 Lakini Waisraeli waliendelea kuwa na nguvu kwa sababu Mungu alikuwa pamoja nao. Farao alikasirika. Alikuwa na mpango mwingine. Ulikuwa mpango mbaya sana. Aliamrisha kwamba watoto wachanga wavulana wa Waisraeli wote, lazima wauwawe.

Amramu na Yokebedi walikuwa Waisraeli. Walikuwa na mwana aliyeitwa Haruni na binti aliyeitwa Miriamu. Yokebedi alikuwa anatarajia motto mwingine. Waliposikia amri mpya ya Farao, waliogopa sana.

Mtoto mchanga wa Yokebedi alionekana mrembo sana. Yokebedi alimpenda sana. Hakutaka auawe. Kwa hivyo alimficha.

Yokebedi alificha mtoto kwa miezi mitatu. Lakini kila wakati aliogopa kwamba askari wa Farao wangekuja na wamuue. Mtoto alipokua mkubwa alikuwa akilia na kufanya kelele. Yokebedi alijua kwamba hangeendelea kumficha.

12.3 Usiku moja Yokebedi alitengeneza kikapu cha majani. Alifunika kile kikapu kwa lami kuzudi maji yasiingie ndani. Asubuhi yake aliweka mtoto kwa kikapu na akampeleka na kumficha kando ya mto ndani ya unyasi. Yokebedi aliambia bintiye Miriamu aende kujificha ndani ya unyasi ili aangalie mtoto.

Binti wa Farao alishuka chini kwa mtoni ili aoge. Binti alisikia mtoto akilia. Aliona kikapu kimefichwa ndani ya unyasi. Binti alituma mjakazi wake aende achukue kile kikapu.

Binti alipoona mtoto mvulana mzuri, aliamua kumchukua huyo mtoto. Lakini alitaka yaya wa kumlea mpaka atakapokua mkubwa.

Miriamu alikuwa anaangalia. Aliona binti mfalme akimuokota kakake mchanga. Alifurahi aliposikia kwamba binti Farao alitaka kumchukua. Alijua kwamba binti Farao atataka mtu wa kumlelea huyo kakake mchanga.

Miriamu alikimbia kwa binti mfalme. Akamuuliza, “Niende nikuletee mwanamke Mwisreali akulelee mtoto?” Binti Farao alijibu,”Ndiyo nenda.” Miriamu alikimbia na kumleta mama yake.

12.4 Binti Farao alimpa Yokebedi huyo mtoto na akamwambia amlelee. Binti Farao alikuwa akimlipa Yokebedi mshahara wa kulea mtoto. Yokebedi alirudishiwa mtoto wake akiwa mzima na kwa salama – na alikuwa akilipwa kwa kumlea. Yokebedi alifurahi sana asana. Alishukuru Mungu kwa kumwokoa mwanawe.

Mtoto alipokua mkubwa, Yokebedi alimpeleka kwa binti Farao na akawa mwanawe. Binti Farao alimwita MUSA, kumaanisha ‘okoa kutoka kwa maji,’ kwa sababu aliokoa maisha yake alipompata kwa unyasi kando ya mto.

Musa alikua mkubwa kwa jumba ya mfalme akiwa na binti Farao. Lakini hakusahau familia yake ya halali.